

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO



MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA AROBAINI NA SITA

17 JUNI, 2022



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA AROBAINI NA SITA – TAREHE 17 JUNI, 2022

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

401. **MHESHIMIWA FRANCIS LEONARD MTEGA (MBARALI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Mamlaka ya Mji Mdogo wa Rujewa itakuwa Mamlaka kamili.

402. **MHESHIMIWA SIMON SONGE LUSENGEKILE (BUSEGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini ahadi ya Rais wa Awamu ya Tano ya kuipandisha hadhi Shule ya Sekondari Nassa kuwa ya Kidato cha Tano na Sita itatekelezwa.

403. MHESHIMIWA JAQUELINE KAINJA ANDREW (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha kukamilisha ujenzi wa Shule katika Kijiji cha Izingabatogilwe Kata ya Ugalla - Urambo.



WIZARA YA MAJI:

404. MHESHIMIWA SALMA RASHID KIKWETE (MCHINGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itapeleka maji katika Jimbo la Mchinga kutoka kwenye chanzo cha maji cha Ng'apa.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

405. MHESHIMIWA MOHAMED JUMAH SOUD (DONGE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni Vigezo gani hutumika kuanzisha Vituo vya Polisi maeneo yenye idadi kubwa ya watu pamoja na vitendo vya uhalifu.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

406. MHESHIMIWA DKT. FAUSTINE ENGELBERT NDUGULILE (KIGAMBONI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni kiasi gani cha fedha kimekusanywa tangu Daraja la Nyerere lianze kutumika na ni lini huduma ya daraja hili itatolewa bila malipo.

407. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINA CHRISTOPHER MNZAVA (VITI MAALUM):


Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya kutoka Old Shinyanga kupitia Iselamagazi, Solwa hadi Salawe kwa kiwango cha lami.

408. MHESHIMIWA KABULA ENOCK SHITOBELA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itapunguza Tozo zinazotozwa na TPA kwani imekua ikitoza Tozo kubwa kwenye mizigo kuliko Makampuni binafsi.



WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:



409. MHESHIMIWA ALLY MOHAMED KASSINGE (KILWA KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, ni lini Serikali itafanya marekebisho ya Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2020 ambazo zinalalamikiwa na Wadau wa Sekta ya Uvuvi.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

410. MHESHIMIWA NASHON WILLIAM BIDYANGUZE (KIGOMA KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, ni lini Serikali itajenga Mahakama ya Wilaya Uvinza.

III. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2022 (The Finance Bill, 2022).

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Kwamba, Bunge sasa likubali Kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2021 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Kwamba, Bunge sasa likubali Kupokea na Kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
17 JUNI, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**

